



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA

MAELEKEZO MAHSUSI YA USAILI

1. Tume ya Utumishi wa Mahakama inawatangazia waombaji wote waliomba nafasi za kazi na kufanikiwa kupata nafasi ya kuingia kwenye kundi la kufanya usaili (**Shortlisted Candidates**) kuwa, usaili utafanyika katika awamu mbili au tatu kutegemeana na kada husika kama ifutavyo:-
 - i. Usaili wa kuandika kwenye kompyuta - Waombaji wote
 - ii. Usaili wa ana kwa ana (**Oral Interview**) waombaji watakaoshinda Usaili wa kwanza (Majibu ya Usaili wa kwanza yatatoka siku hiyo hiyo ya usaili)
 - iii. Usaili wa vitendo (**Practicals**) - Kada za Mahakimu, madereva na makatibu Muhtasi (Maelekezo yatatolewa kwa washindi wa usaili wa wa kwanza).
2. Tume imeweka utaratibu wa maeneo ya kufanya usaili **katika mikoa sita (6)** ambayo ni **Dar es salaam (DIT); Morogoro (Mahakama Kuu); Mbeya (Mahakama Kuu); Dodoma (Mahakama Kuu); Mwanza (Mahakama Kuu) na Arusha (Mahakama Kuu)**.
3. Wasailiwa wote 713 watatakiwa kufanya usaili wa awamu ya kwanza **kwa kutumia kompyuta (Computer-based written interview)** ambao utafanyika katika Ofisi za Mahakama Kuu za Mikoa husika Isipokuwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam watafanya usaili huo katika Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam (DIT). Muda wa kuanza usaili kwa vituo vyote utakuwa **saa 2:00 asubuhi**. Unashauriwa kuja na komputa mpakato '**laptop**', yenyе akiba ya umeme inayoweza kudumu kwa **saa moja** au zaidi , ila kama huna utaratibu utafanyika kwa ajili ya kukuwezesha kufanya usaili kwa kutumia kompyuta.

4. **Waombaji kada ya Mahakimu**, watafanya usaili **wa aina tatu** kama ifuatavyo:-

 - a. **Usaili kwa kutumia kompyuta (Computer-based written interview)** utafanyika Mkoani Dar es salaam katika Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam (DIT) tarehe **15 Juni, 2022**, kuanzia saa **2.00 asubuhi** ;
 - b. Kwa waombaji watakaoshinda usaili wa tarehe 15 Juni, 2022 watapata sifa ya kuitwa kufanya Usaili wa **kujibu maswali kwa kuandika kwenye karatasi (paper-based written Interview)** katika Chuo Cha Utumishi wa Umma (TPSC- Magogoni). Hatimaye kufuatiwa na **usaili wa ana kwa ana (Oral Interview)** utakaofanyika katika Ofisi za Tume ya Utumishi wa Mahakama zilizopo Mtaa wa Lithuli – Haki House tarehe **16 na 17 Juni 2022**.
5. **Waombaji kada ya Dereva II na Katibu Mahsusii III watakaoshinda Usaili wa kwanza** watapata sifa ya kufanya **usaili wa vitendo (Practicals)** utakaofanyika Dar es salaam katika **Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)** na Chuo Cha Utumishi wa Umma (TPSC- Magogoni) Mtawalia, **tarehe 17 Juni,2022**. Aidha usaili wa ana kwa ana (Oral Interview) utafanyika **tarehe 18 Juni,2022** katika Ofisi za Tume, Haki House kuanzia saa **2.00 asubuhi**.
6. Waombaji wa Kada ya **Afisa Utumishi II; Afisa Tawala II; Msaidizi wa Kumbukumbu II; Msaidizi wa Hesabu II; Afisa Hesabu II na Afisa Mkaguzi wa Ndani II** watakaoshinda Usaili wa kwanza watapata sifa ya kuitwa kufanya usaili wa ana kwa ana (Oral Interview) **tarehe16 Juni, 2022** katika vituo walikofanyia usaili wa kwanza. Kwa Dar es salaam usaili utafanyika katika Ofisi za Tume ya Utumishi wa Mahakama, Haki House, Mtaa wa Lithuli.
7. Wasailiwa wote waainishe wenyewe Mkoa watakaofanyia usaili kupitia email zifuatazo;- Dar es salaam (daressalam.zone@jsc.go.tz), Morogoro (morogoro.zone@jsc.go.tz), Dodoma (dodoma.zone@jsc.go.tz), Arusha (arusha.zone@jsc.go.tz) Mwanza (Mwanza.zone@jsc.go.tz), Mbeya (Mbeya.zone@jsc.go.tz). Aidha wasailiwa wanasisitizwa waje na vyeti halisi vya shule na vya taaluma pamoja na kitambulisho chenye picha.
8. Mwisho, mnakumbushwa kutembelea tovuti ya Tume (www.jsc.go.tz) na ya Mahakama (www.judiciary.go.tz) mara kwa mara ili kupata taarifa na maelekezo mengine. Kwa

maulizo ya simu piga namba 0734-219821 (saa 24), barua pepe maulizo.ajira@jsc.go.tz.
Ili kuwezesha uhakiki, fika kwenye kituo cha usaili kuanzia saa moja asubuhi.

Imetolewa na;

Prof. Elisante Ole Gabriel.

KATIBU

TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA